

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



MKUTANO WA SITA

KIKAO CHA KUMI NA NNE

18 FEBRUARI, 2022



## ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

### MKUTANO WA SITA

**KIKAO CHA KUMI NA NNE – TAREHE 18 FEBRUARI, 2022**

**I. DUA:**

**II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:**

**WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI:**

Taarifa ya Mwaka na Hesabu zilizokaguliwa za Mfuko wa Barabara kwa Mwaka wa Fedha ulioshia tarehe 30 Juni, 2020 (*The Annual Report and Audited Accounts of the Roads Fund Board for the Financial Year ended 30<sup>th</sup> June, 2020*).



**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:**

Maelezo ya Waziri wa Fedha na Mipango kuhusu Mapendelekezo ya Nyongeza ya Bajeti ya Mwaka 2021/2022.

## **MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti kuhusu Mapendekezo ya Nyongeza ya Bajeti ya Mwaka 2021/2022.

## **MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA SHERIA NDOGO:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2021.

### **III. MASWALI:**

#### **OFISI YA WAZIRI MKUU:**

#### **159. MHESHIMIWA MUSSA RAMADHANI SIMA (SINGIDA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kutoa muongozo kwa Vyama vya Wafanyakazi hasa Chama cha Walimu Tanzania (CWT) na kupunguza ada ya Uanachama au kuondoa kabisa mfumo wa asilimia ili kuweka kiwango kitakachokubaliwa na Wanachama wenyewe.

## **OFISI YA RAIS (TAMISEMI):**

### **160. MHESHIMIWA DKT. CHRISTINE GABRIEL ISHENGOMA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, Serikali ina mpango gani wa kutatua tatizo la upungufu wa Wataalamu wa Afya hasa Manesi katika Vituo vya Afya na Zahanati Mkoani Morogoro.

### **161. MHESHIMIWA DAUD PROTAS VENANT (IGALULA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kumalizia Maboma yaliyojengwa kwa nguvu za Wananchi kwa ajili ya Elimu, Afya na Polisi.

## **WIZARA YA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA:**

### **162. MHESHIMIWA TIMOTHEO PAUL MNZAVA (KOROGWE VIJIJINI):**


Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kufufua Kiwanda cha Tembo Chipboard kilichopo Kata ya Mkumbara Wilayani Korogwe.

## **WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:**

### **163. MHESHIMIWA ANGELINA ADAM MALEMBEKA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:-



Je, ni Wanyama wa aina gani wanaruhusiwa kufugwa na utaratibu gani unaotumika kuwapata na Serikali ina mkakati gani kuhakikisha Wanyama hao hawasafirishwi kwenda nje ya nchi.

### **164. MHESHIMIWA ABEID IGHONDO RAMADHANI (SINGIDA KASKAZINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:-

Je, mchakato wa Serikali kukamilisha zoezi la Msitu wa Mgori kuwa Hifadhi ya Taifa umefikia wapi na ni faida gani Wananchi watazipata kwa msitu huu kuwa Hifadhi.

## **WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLIJIA:**

### **165. MHESHIMIWA EDWIN ENOSY SWALLE (LUPEMBE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia:-

Je, kuna changamoto gani katika kukuza na kuendeleza Mfuko wa Elimu na Bodi ya Mikopo ili kukopesha Wanafunzi wengi zaidi.

## **WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**

### **166. MHESHIMIWA DKT. RITTA ENESPER KABATI (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, ni lini Serikali itatekeleza ahadi yake ya kuhamisha Gereza la Mkoa wa Iringa ili kuondoa muingiliano uliopo kati ya Gereza hilo na Hospitali ya Mkoa wa Iringa.

### **167. MHESHIMIWA NICHOLAUS GEORGE NGASSA (IGUNGA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, ni lini Serikali itafanya ukarabati wa nyumba za makazi ya Askari wa Jeshi la Polisi kwenye Kituo cha Polisi cha Wilaya ya Igunga.

### **WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI:**

#### **168. MHESHIMIWA TASKA RESTITUTA MBOGO (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, ni lini Serikali itajenga barabara ya kutoka Mpanda kwenda Karema kwa kiwango cha lami.

### **WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO:**

#### **169. MHESHIMIWA ENG. EZRA JOHN CHIWELESA (BIHARAMULO MAGHARIBI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango:-

Je, ni lini kiasi cha Shilingi 204 Milioni zilizorejeshwa Hazina Mwaka wa Fedha 2019/2020 zitatolewa kwa ajili ya ujenzi wa Majengo mawili ya Hospitali ya Wilaya ya Biharamulo.

## **WIZARA YA AFYA:**

### **170. MHESHIMIWA KASSIM HASSAN HAJI (MWANAKWEREKWE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:-

Je, ni lini Serikali itaona umuhimu wa kuongeza maduka ya kutolea dawa kwa kutumia Bima ya Afya ili kuondoa usumbufu wanaopata Wananchi wa Zanzibar.

## **WIZARA YA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:**

### **171. MHESHIMIWA SAASHISHA ELINKIYO MAFUWE (HAI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga Kiwanja cha Michezo katika Wilaya ya Hai.

## **IV. HOJA ZA SERIKALI:**

### **WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:**

Kwamba Bunge sasa likubali kupokea na kuitisha Mapendekazo ya Nyongeza ya Bajeti ya Mwaka 2021/2022.

## **V. MUSWADA WA SHERIA YA SERIKALI:**


(Kusomwa Kwa Hatua Zake Zote)

Muswada wa Sheria ya Kuidhinisha Matumizi ya Ziada ya Serikali (Kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022) wa Mwaka 2022 [*The Supplementary Appropriation (For Financial Year 2021/2022) Bill, 2022*].

## **VI. HOJA ZA KAMATI:**

**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA SHERIA NDOGO:**

Kwamba, Bunge sasa lipokee na kukubali Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2021.



## **VII. TAARIFA YA KATIBU WA BUNGE:**



## **VIII. HOJA YA KUAHIRISHA BUNGE:**

**WAZIRI MKUU:**

## **IX. WIMBO WA TAIFA NA WIMBO WA AFRIKA MASHARIKI.**

**DODOMA**

**18 FEBRUARI, 2022**

**N.J. MWIHAMBI, *ndc***

**KATIBU WA BUNGE**